FUNZO LA 11

-Hapo mwanzo, Adamu na Hawa waliishi wapi?
-Katika bustani ya Edeni.

-Katika bustani ya Edeni, Adamu na Hawa walikuwaje?
-Adamu na Hawa walikuwa na furaha sana.

-Kwa nini Adamu na Hawa walikuwa na furaha sana?

-Kwa sababu Adamu na Hawa walitembea na Mungu.
-Kwa sababu Adamu na Hawa walikuwa na kila kitu walichohitaji.

-Lakini Shetani, adui wa Mungu, alikuwa wapi?

-Shetani alikuwa akitazama wakati Mungu aliwaumba Adamu na Hawa.

-Shetani alijua kuwa Mungu aliwaumba Adamu na Hawa kwa mfano wake, na alikasirika sana.

-Shetani alijua kuwa Mungu alimpa Adamu mamlaka juu ya nchi yote, na alikasirika sana.

-Shetani anamchukia Mungu.
-Shetani alijua kuwa hangeweza kumshinda Mungu.

-Kwa hivyo, Shetani aliamua kuwashinda Adamu na Hawa.
-Kwa hivyo, Shetani aliamua kuwaharibu Adamu na Hawa.



-Je, ni jinsi gani Shetani alijaribu kuwaharibu Adamu na Hawa?

Tusome Mwanzo 3:1

1-Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?

-Je, ni nyoka aliyekuwa akizungumza na Hawa?
-La.

-Ni nani aliyekuwa akizungumza na Hawa?
-Shetani.

-Je, Hawa alijua kuwa ni Shetani aliyekuwa akizungumza na yeye?
-La.

-Shetani alikuwa amemwingia nyoka.

-Kwa nini Shetani alimwingia nyoka?
-Ili ajifiche.

-Kwa nini Shetani alijificha ndani ya nyoka?

-Kwa sababu Shetani alitaka kumtega Hawa.
-Kwa sababu Shetani alitaka kumdanganya Hawa.
-Kwa sababu Shetani alitaka kumharibu Hawa.

-Ufuatao ni mfano:

-Wakati mwiindaji anataka kumtega mnyama wa mwituni, je, yeye hujificha ili amtege huyo mnyama?
-Ndiyo.

-Nini hufanyika iwapo hatajificha?
-Hawezi kumtega mnyama.

-Jinsi mwiindaji hujificha ili amtege mnyama, Shetani alijificha ili amtege Hawa.

-Je, hata leo, Shetani hujaribu kuwatega na kuwadanganya watu?
-Ndiyo.

-Je, hivi leo, Shetani hujaribu vipi kuwatega na kuwadanganya watu?

-Kwanza, Shetani huzungumza na sisi katika mawazo yetu.
-Pili, Shetani huzungumza na sisi kupitia watu wengine.
-Tatu, Shetani huzungumza na sisi kupitia mapepo.

-Kwanza, Shetani huzungumza na sisi katika mawazo yetu.

-Wakati mwingine, Shetani huweka mawazo katika akili zetu.

-Tunafikiria kuwa hayo mawazo ni yetu, ila ni mawazo ya Shetani na ameyaweka katika akili zetu.



-Shetani atakuwambia usiliamini neno la Mungu.

-Hilo wazo si la Mungu.
-Hilo wazo liliwekwa katika akili yako na Shetani.

-Pili, Shetani huzungumza na sisi kupitia watu wengine.

-Watu wengine wanaweza kukuwambia usilisikilize neno la Mungu.

-Hilo wazo si la Mungu.
-Hilo wazo ni wazo ambalo Shetani aliweka katika akili za mtu mwingine.

-Watu wengine waweza kukuwambia, “Tuko na imani zetu. Kwa hivyo, hatuitaji hizi imani mpya.”

-Hilo wazo si la Mungu.

-Hilo wazo ni wazo ambalo Shetani aliweka katika akili za mtu mwingine.

-Tatu, Shetani huzungumza na sisi kupitia mapepo.

-Mapepo walizungumza na mababu wenu.

-Mapepo waliwaambia mababu wachome watoto wao katika moto, na wakafanya hivyo.

-Hilo wazo si la Mungu.

-Hilo wazo liliwekwa katika akili za mababu wenu na Shetani pamoja na mapepo wake.

-Je, Hawa alijua kuwa ni Shetani aliyezungumza na yeye?
-La.

-Hawa hakujua kuwa ni Shetani aliyezungumza na yeye.
-Kwa sababu Shetani alikuwa amejificha.

-Mababu wenu hawakujua kuwa ni Shetani aliyekuwa akizungumza nao.
-Kwa sababu Shetani alikuwa amejificha.

-Shetani alijificha ili amtege na kumdanganya Hawa.
-Shetani alijificha ili awatege na kuwadanganya mababu wenu.

-Kwa nini Shetani alitaka kumtega na kumdanganya Hawa?

-Kwa sababu Shetani alimchukia Hawa.
-Kwa sababu Shetani alitaka kumharibu Hawa.

-Kwa nini Shetani alitaka kuwatega na kuwadanganya mababu wenu?

-Kwa sababu Shetani anawachukia watu wote.
-Kwa sababu Shetani anataka kuwaharibu watu wote.

-Tusome tena swali ambalo Shetani alimuuliza Hawa.

Tusome Mwanzo 3:1



1-Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani

-Kwa nini Shetani alimuuliza Hawa swali hili?

-Shetani alijua kile Mungu alikuwa amesema.
-Shetani alijua kuwa Mungu alikuwa amewaambia wasile matunda kutoka kwa mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya.

-Kwa nini Shetani alimuuliza Hawa swali hili?

-Shetani alimuuliza Hawa hili swali ili amtege Hawa.
-Shetani alimuuliza Hawa hili swali ili amdanganye Hawa.
-Shetani alimuuliza Hawa hili swali ili amharibu Hawa.

-Tusome jibu la Hawa:

Tusome Mwanzo 3:2-3

2-Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula;
3-lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.

-Mungu hakusema kuwa Adamu na Hawa wasiguze hilo tunda.

-Mungu alisema tu, Adamu na Hawa wasile hilo tunda.

-Katika kitabu cha Mungu, tunasoma kuwa Mungu alimuamuru Adamu pekee asile hilo Tunda.

-Ila amri ya Mungu kwa Adamu, ilikuwa pia amri ya Mungu kwa Hawa.

-Ijapokuwa Maneno ya Mungu yaliandikiwa watu walioishi miaka mingi iliyopita, pia Maneno ya Mungu yameandikiwa sisi tunaoishi sasa.

-Mungu hana ujumbe mmoja kwa watu weusi, na ujumbe mwingine kwa watu weupe.

-Mungu hana ujumbe mmoja kwa Waafrika, Na ujumbe tofauti kwa wazungu.

-Ujumbe wa Mungu ni sawa kwa watu wote.
-Ujumbe wa Mungu ni sawa jana, leo na hata milele.

-Je, Shetani alimjibu vipi Hawa?

Tusome Mwanzo 3:4-5

4-Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa,
5-kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.

-Je, Mungu alimwambia Adamu nini kingefanyika kama wangekula kutoka kwa mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya?



-Wangekufa.

-Je, Shetani alimwambia Hawa nini kingefanyika kama wangekula kutoka kwa mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya?
-Hawangekufa.

-Mungu alisema kuwa Adamu na Hawa wangekufa kama wangekula hilo tunda.

-Shetani alisema kuwa Adamu na Hawa hawangekufa kama wangekula hilo tunda.

-Je, ni nani aliyekuwa akisema ukweli, Mungu au Shetani?
-Mungu.

-Je, Shetani alikuwa anamuita Mungu nini?
-Shetani alikuwa anamuita Mungu mdanganyifu.

-Ni nini kingine Shetani alimwambia Hawa kingefanyika kama angekula kutoka kwa mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya?

-Shetani alisema wangekuwa kama Mungu.

-Je, watu wanaweza kuwa kama Mungu?
-La.

-Ni Mungu pekee ndiye Mungu.

-Shetani alikuwa anamdanganya Hawa alipomwambia kuwa angekuwa kama Mungu.

-Hapo mwanzo, Shetani hakumtii Mungu.
-Sasa, Shetani alitaka Hawa asimtii Mungu.

-Mungu hakuwaumba watu ili waishi jinsi watu wanavyosema.
-Mungu aliwaumba watu ili waishi jinsi Mungu anavyosema.

-Mungu hakuwaumba watu waishi katika masharti yao.
-Mungu aliwaumba watu waishi katika masharti ya Mungu.

-Je, Hawa alifanya nini?
-Hawa alimtii Mungu?

Tusome Mwanzo 3:6

6-Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.

-Shetani alimdanganya Hawa, na Hawa alimwamini Shetani.

-Hawa hakumtii Mungu, na akala lile tunda.
-Adamu pia hakumtii Mungu, na akala lile tunda.

-Adamu na Hawa walimsikiliza Shetani.
-Adamu na Hawa hawakumsikiliza Mungu.

-Adamu na Hawa hawakumtii Mungu.
-Adamu na Hawa walitenda dhambi kwa Mungu.



-Kwa sababu Adamu na Hawa hawakumtii Mungu, wakawa adui wa Mungu.

-Kwa sababu Adamu na Hawa walimsikiliza Shetani, wakawa maadui wa Mungu.

-Ufuatao ni mfano:

-Kama rafiki yako angekuwacha na aanze kumfuata adui yako, ambaye alitaka kukuua, je, rafiki yako angekuwa adui yako?
-Ndiyo.

-Kwa sababu Adamu na Hawa walimuacha Mungu, Wakawa adui wa Mungu.

-Kwa sababu Adamu na Hawa walimfuata Shetani, wakawa maadui wa Mungu.

-Nini kingine kilifanyika baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi?

Tusome Mwanzo 3:7-8

7-Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo.
8-Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone.

-Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, walitambua nini?

-Walitambua kuwa walikuwa uchi.

-Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, walifanya nini walipotambua kuwa walikuwa uchi?

-Walijifanyia mavazi kutoka kwa majani.

-Baada ya Adamu na Hawa kutenda Dhambi, walifanya nini walipomsikia Mungu akija kuwaona?

-Walijificha kutoka kwa Mungu.

-Je, yawezekana kujificha kutoka kwa Mungu?
-La.

-Kwa nini haiwezekani kujificha kutoka kwa Mungu?
-Mungu yuko kila mahali.

-Awali, Adamu na Hawa walikuwa marafiki wa Mungu.
-Sasa, Adamu na Hawa wakawa maadui wa Mungu.

-Awali, Adamu na Hawa walikuwa watoto wa Mungu.
-Sasa, Adamu na Hawa wakawa watoto wa Shetani.

-Awali, Adamu na Hawa walitembea na Mungu.
-Sasa, Adamu na Hawa wakajificha kutoka kwa Mungu.

-Awali, Adamu na Hawa walimfuata Mungu.
-Sasa, Adamu na Hawa walimfuata Shetani.



-Awali, Adamu na Hawa hawakujua dhambi.
-Sasa, Adamu na Hawa walijua dhambi.

-Awali, Adamu na Hawa hawakuona aibu.
-Sasa, Adamu na Hawa wakawa na aibu.

-Shetani anamchukia nani?
-Shetani anamchukia Mungu na watu wote.

-Shetani anamchukia Mungu, na anajaribu kuharibu kazi za Mungu.
-Shetani anawachukia watu wote, na anajaribu kuharibu watu wote.

-Je, Shetani anataka usikilize neno la Mungu?
-La.
-Kwa nini Shetani hataki usikilize neno la Mungu?

-Kwa sababu Shetani anawachukia watu wote, na anawataka waende katika Ziwa la Moto wa Milele.

-Ukilisikiliza Neno la Mungu, waweza kujifundisha jinsi ya kuepuka Ziwa la Moto wa Milele.

-Kama hutasikiliza Neno la Mungu, hautajifundisha jinsi ya kuepuka Ziwa la Moto wa Milele.

-Mungu anataka usikilize neno lake.
-Shetani hataki usikilize Neno la Mungu.
-Natumai utasikiliza Neno la Mungu.